https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness



https://www.path-2-happiness.com/sw

# NJIA IKO WAPI?!

https://www.path-2-happiness.com/sw

# Yaliyomo

NJIA IKO WAPI?!

Watu wote wanatafuta furaha, njia iko wapi?!

Je, ni Njia ya Kumkana Mungu au Njia ya Dini?

Kuna maswali ambayo bado yanahitaji majibu

Majibu yawe vipi?

Dalili ni zipi?

Dalili za uungu wa Allah ta'ala



https://www.path-2-happiness.com/sw



# NJIA IKO WAPI?!

## Watu wote wanatafuta furaha, njia iko wapi?!


https://www.path-2-happiness.com/sw

Watu wote wanatafuta furaha, hivyo basi njia iko wapi?! Kila mtu kwa njia yake nyepesi anatafuta furaha, pamoja na tofauti mbalimbali za watu kuhusu madhehebu yao, kabila zao, utaifa wao, misingi yao ya kimaadili, malengo yao, ila wote kwa pamoja wanaafikiana katika lengo moja; nayo ni; kutafuta furaha na utulivu.

Utakapomuuliza mtu yeyote: Kwa nini unafanya hivi? Na kwa nini umefanya vile? Atajibu: Nataka furaha!! Awe amesema hivyo moja kwa moja au kwa maana yake.

Kama ni hivyo ni nini furaha, na tunawezaje kuifikia?!

Furaha ni hisia za utulivu inayoendelea, yenye raha, tumaini na shangwe, hisia hizi hutokea kwa matokeo ya hisia ya mambo matatu yenye kudumu, nayo ni; wema wa dhati ya mtu, wema wa maisha ya mtu, na wema wa mwisho wa mtu.



### Furaha kwa mkabala

“Huenda ukasimamia jambo lisilokuletea furaha lakini hakuna furaha bila ya kusimamia jambo.”

**Benjamin Disraeli**

*Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza.*



### Furaha ipo karibu sana na sisi

“Tunaitafuta furaha mara nyingi lakini ipo karibu yetu, kama vile tunavyotafuta miwani iliyopo machoni mwetu.”

**Tolstoy**

*Mwanafasihi wa Urusi*

Kuhusu mambo haya matatu mtu huanza kujiuliza mwenyewe, na maswali yanaongezeka na kuwa makubwa kila akikua, wala mtu huyo hapati furaha hadi aweze kujibu maswali yake yanayomjia mara kwa mara akilini, miongoni mwa maswali hayo ni:-

-Nani mwenye kuumiliki ulimwengu huu na kuufanya atakavyo?

-Ni nani aliyeniumba na kuumba ulimwengu huu ulionizunguka?

-Mimi ni nani? Nimetoka wapi? Kwa nini nimeumbwa? Mwisho wangu uko wapi.

Pindi mwamko wa mwanadamu unapozidi katika nafsi yake na katika maisha yake, maswali haya huzidi kumsumbua akilini mara kwa mara, kwenye fikra zake na roho yake, wala hapati utulivu wowote na furaha hadi zipate majibu yake na kutuliza nafsi yake.

**Njia zimekuwa nyingi**
**Mungu ni mmoja**

"Ikiwa hujui unakwenda wapi, basi njia zote zitakupeleka huko."



**Lewis Carol**
Mwana Hisabati

## Je, ni Njia ya Kumkana Mungu au Njia ya Dini?

Watu huanza kufikiria kujibu maswali yaliyotangulia, kuna njia mbili; Njia ya kwanza ni ile ya kumkana Mungu, na ya kuwa ulimwengu ni maada.


Njia ya pili ni ile ya kumuamini Mungu kuwa ni Muumba wa kila kitu; na matokeo yake ni kujitokeza kwa maswali mengi miongoni mwake ni:-

-Je, inawezekana ulimwengu ukapatikana wenyewe tokea hapo mwanzo kutokana na maingiliano yaliyokuja ghafla bila kupangiwa muda.

-Je, inaingia akilini kuwa ghafla hii ya bahati nasibu isiyokuwa na mpangilio wowote ndio imeupata ulimwengu huu ulioratibiwa vizuri?!!

-Je, alichofikia mwanadamu tokea apatikane katika historia nzima ni zao la ukuzi au ndio huo ughafla wa bahati nasibu?!! Na ya kuwa sisi ni unyoya katika pepo yenye kuugeuza geuza kwa hali hiyo hiyo ya ghafla na fujo?!!

https://www.path-2-happiness.com/sw



**Ainisha Muelekeo wako**

"Kwa hakika ulimwengu unakunjua njia kwa ajili ya mwenye kujua anakokwenda."

**Ralph Waldo Emerson**
Mwanafalsafa wa Kimarekani

-Je, mwanadamu ndio Mungu aliyepanga sheria, nae ni Muumba mbunifu, naye ni kila kitu, na nyuma yake hamna kitu kingine?

-Je, yaliyokuwa nyuma ya maumbile katika mambo ya ghaib. Je ni mazigazi ambayo yanapaswa kupotea mbele ya wasio kuwa na Dini na Ulimwengu wa maada?.

-Je, mwanadamu ni maada tu asiyekuwa na mazingatio yoyote, au ni kuwa asili yake ilikuwa ni nyani aliyeendelea kwa kupita muda?


Ni aina gani maada ya ambayo inaweza kumuumba mwanadamu mwenye sifa hizi za hali ya juu, na mengi bora matukufu, aliyeumbwa kwa mengi ya kushangaza?!

Na je asiyekuwa nacho anaweza kutoa?!

-Je, dunia ndio lengo la mwanadamu na mwisho wa kimbilio lake, hakuna mazingatio kwa yaliyosemwa na dini mbali mbali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwepo nguvu nyingine zisizokuwa mwanadamu, au maisha mengine yasiokuwa maisha haya?

Allah Ta'ala amesema kuhusu kufikiri kwa watu hao. {Na walisema: Hapana ila huu uhai wetu wa duniani - twafa na twaishi, na hapana kinacho tuhiliki isipo kuwa dahari. Lakini wao hawana ilimu ya hayo, ila wao wanadhani tu.} [45:24],

Kuhusu wale waliokataa na kupinga Allah Ta'ala amesema, {Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo. Basi angalia ulikuwaje mwisho wa mafisadi!} [27:14].



**Einstein**
Mwanazuoni wa Fizikia

**Elimu na Dini**

"Mimi si amini ya kuwa elimu yapasa igongane na dini katika hali ya kawaida. Kwa hakika ninaona kuna uhusiano na fungamano baina yao. Hivyo basi mnasema kuwa elimu bila ya dini ni kama vile mtu aliyepooza mguu. Na dini bila ya elimu ni kipofu kila kimoja ni muhimu. Zinatakiwa zifanye kazi pamoja mkono kwa mkono. Inaelekea kwangu kuwa Yule ambae hatofurahishwa na ukweli katika elimu na dini ni kama mtu aliyekufa."



https://www.path-2-happiness.com/sw



**Newton**
Mwanafalsafa wa Uingereza

## Ulahidi (Kumkana Mungu)... ni aina ya Upumbavu

"Kumkana Mungu ni aina ya Upumbavu: Ninapoangalia utaratibu wa jua ninaona kuwa ardhi imekaa sehemu inayostahiki kutoka kwenye jua, ambayo inayoiwezesha kupata kiasi cha kutosha cha joto na mwanga, na hii bila ya shaka halijatokea ghafla."

Kwa hakika wapinga dini (walahidi) wanakiri udhaifu wao kamilifu kuhusu

kujua siri ya uwepo wa uhai kwa kiumbe chochote; vyovyote awavyo, awe ni mdogo kwa umbile au mkubwa, na wanakiri kuwa hawawezi kurejesha roho kwa mtu kama imefika kooni, kama ni hivyo ipo wapi ile maada wanayoiona kuwa ndio iliyopata na kuwepo ndani ya ulimwengu huu?!

Ni maada gani iliyotumika katika kupatisha ulimwengu huu?!


Na kwa nini wasiweze kuifikia ili kurejesha roho baada ya kiwiliwili kuwa maada isiyo na uhai wowote?.

Ikiwa kinachosemwa na hawa wanaopinga uwepo wa Mwenyezi Mungu ni sahihi iweje basi binadamu wote wakakubaliana kuheshimu dini kiasi hiki.

Kinachosemwa na hawa wapinzani wa Mwenyezi Mungu ya kuwa dini ni ndoto na mambo tu ya kufikirika?!

Kama ni hivyo kwa nini Mitume katika zama zao waliweza kubakisha mafundisho yao hai katika mioyo ya watu, wakati ambapo fikra mbali mbali za watu zimesahaulika, bali si hivyo tu, zimechuja baada ya kupita muda pamoja na njia mbali mbali za kuvutia zinazotumiwa na watu na ufasaha wao?!

Inawezekana vipi kutofautisha baina ya matendo ya kheri na yale ya shari? Bali ni kitu gani ambacho kinaweza kumkataza na kumzuia jambazi kuekeleza ujambazi wake? Na kitu gani kinaweza kufanya moyo wa



**Plato**
Mwanafalsafa wa Kigiriki (Kiyunani)

## Ni nzuri yenye kufuata mfumo maalumu

"Kwa hakika Ulimwengu ni dalili katika uzuri na nidhamu wala hilo haliwezi kuwa ni matokeo ya sababu ya Itifaki, bali ni umbile la mwenye akili mwenye kukusudia kheri na kupanga kila kitu kwa makusudio na hekima."

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



## Furaha ya Kweli

"Hivi sasa ninaishi katika uhalisia na sio katika haiba ile ya udanganyifu ambayo tunaishi katika maisha yetu ya sasa. Maada, matumizi yetu, na maingiliano yetu na jinsia nyingine pamoja na matumizi ya mihadarati. kwa kudhania kuwa hivi ndivyo vinavyotupa furaha lakini kwa sasa nimeona Ulimwengu uliojaa furaha na uliojitosheleza kwa upendo, matarajio na amani.

**Lauren Booth**

Mwanaharakati wa haki za binaadamu wa Uingereza

tajiri kumhurumia fukara? Na kipi kinaweza kumzuia mwizi na mtu mwenye kughushi, haini na mlevi wa

mihadarati..wote hawa kipi kinachoweza kuwazuia kutekeleza matamanio yao?

Kwa hakika jamii za wakana Mungu zinaishi pamoja kama vile makundi ya mbwa mwitu yanayoishi kati ya wenye kudhulumu, wabinafsi, wenye kujipendelea, mapenzi ya matamanio yao na mengineyo; na hivyo basi ukanaji wa Mungu ni sababu kubwa ya tabu azipatazo mwanadamu, ufakiri, kuzidi kwa chuki, hofu na wasiwasi, amesema Allah Mtukufu: {Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu.} [20:124].

Ukanaji Mungu ni fikra batili ambavyo akili, mantiki wala maumbile hayakubali, ni fikra batili inayopingana na elimu; na ndio maana wanazuoni wengi wamewapinga, kama ambavyo inakwenda kinyume na mantiki, kwani fikra yake imesimamia kuwa katika maisha haya hakuna mantiki, bali ni suala la ghafla na bahati nasibu tu ndio iliyouanzisha ulimwengu huu mzuri, wala hakuna maumbile maalum yaliyouanzisha; maumbile sahihi ni yale yanayomlingania mtu kuwa na dini hata kwa wale wanaojidai kuwa hawaamini: {Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo. Basi angalia ulikuwaje mwisho wa mafisadi!} [27:14].

https://www.path-2-happiness.com/sw

# KUNA MASWALI AMBAYO BADO YANAHITAJI MAJIBU


Bila elimu mwanadamu anakuwa si mwenye kufahamu majibu ya maswali haya, wala elimu za kisasa hazijaweza kujibu maswali haya; kwani kadhia hizi zinaingia katika mzunguko wa dini; na kwa ajili hiyo riwaya zimekuwa nyingi na ushirikina na simulizi zimekuwa nyingi katika maswali haya; jambo ambalo linazidisha babaiko kwa mwanadamu na kumtia hofu.

Wala mwanadamu hawezi kusimama kujibu majibu yenye kutosheleza kwa maswali hayo ila atakapoongozwa na Allah katika njia sahihi ambayo itamfikisha katika wema, amani na utulivu na kwenye furaha na raha.

Kadhia hizi na maswali haya hayaelezwi na kufafanuliwa na mfano wake ila kwenye dini mbali mbali; kwa sababu kadhia hizi huchukuliwa na kuzingatiwa kuwa ni katika elimu za mambo ya ghaibu, na dini iliyokuwa sahihi ndio ambayo inajipwekesha na haki na kauli ya kweli; kwa sababu ni kutoka kwa Allah ambaye amewapelekea wahyi Mitume wake, amesema Allah Ta'ala: {…Sema: Hakika uwongofu wa Mwenyezi Mungu ndio uwongofu…}[2:120]

Na kauli yake Allah: {…Sema: Hakika uwongofu ni uwongofu wa Mwenyezi Mungu…} [3:73]

Hivyo basi imekuwa ni lazima kwa mwanadamu kuikusudia dini ya haki, kujifunza na kuiamini; ili babaiko hili na shaka limuondoke, na aelekee katika njia iliyonyooka, njia ya furaha na ya tumaini.



## Ifanye furaha kuwa ni lengo lako

"Ukitaka kuwa mwenye furaha: Unganisha furaha na lengo na sio na mtu au na kitu."

**Einstein**
Mwanazuoni wa Fizikia

https://www.path-2-happiness.com/sw



## MAJIBU YAWE VIPI?!

Allah amesema: {Na kwa yakini tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo. Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti. Kisha tukaiumba tone kuwa damu iliyo ganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama. Kisha tukamfanya kiumbe mwengine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji. Kisha hakika nyinyi baada ya hayo mtakufa. Kisha hakika nyinyi Siku ya Kiyama mtafufuliwa.} [23:12-16].

Hivyo basi mwisho wa kimbilio letu ni kufafanuliwa na kurudi kwetu kwa Allah Ta'ala, kwa maana hiyo maumbile haya hayakuwa ni mchezo (Mwenyezi Mungu Ametukuka dhidi ya kufanya mchezo) bali yalikuwa yenye hekima kubwa, Allah amesema: {Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa?} [23:115].

Hiyo basi Allah hakuuumba mwanadamu na majini kwa mchezo, bali amewaumba kwa kumuabudu yeye peke yake tu bila kumshirikisha na yeyote, kumuabudu yeye tu kwa mtazamo mpana kwa kufanya yote ayapendayo Allah Ta'ala na kuridhika katika aliyoyafaradhisha, na swala, na dhikri na kuimarisha ardhi, na kuwanufaisha watu; Allah amesema: {Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi.} [51:56]

Watu wote wanarejea na kukimbilia kwake tu, pamoja na marejeo yote ni kwake; Allah amesema: {…Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu...} [3:28].

Yakini inaondosha mchezo katika maisha ya watu, na kuwapa maana ya maisha yao, na furaha katika mioyo na roho zao Allah amesema: {Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji? Au wao wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana na yakini. } [52:35-36]



**Descartes**

Mwanafalsafa wa Kifaransa

### Muumba wa Kila Kitu

"Mimi nipo: Basi ni nani aliyenileta na ni aliyeniumba?, Mimi sijajiumba; hapana budi kuwepo na Muumba, na Muumba huyu hapana budi awe wajibu wa uwepo. Asiyehitaji uwepo wa mwingine aliyemleta, au mwenye kuhifadhi uwepo wake, Mungu huyu anapasa kusifika kwa sifa zote za uzuri Muumba huyu ni Allah mwanzilishi wa kila kitu."

https://www.path-2-happiness.com/sw




Mwanadamu anaposhindwa kujua siri ya Ulimwengu huu, na kuanza kufikiria viumbe wa Allah, ardhi, nyota, sayari mbali mbali, mfuatano wa usiku na mchana, uhai na mauti, na yote aliyoyaweka Allah katika Ulimwengu huu…. Mwanadamu akifanya hivyo anafahamu kwa yakini kwa maumbile yake ya asili (fitra) kuwa yupo mtukufu na mkubwa aliyeipata ulimwengu huu ambaye ndie mwenye nguvu zaidi kumshinda yeye, ambaye yeye binadamu anastahiki kunyenyekea kwake, kumuabudu, kutarajia thawabu zake na kuhofia adhabu zake.

Vivyo hivyo tafakuri hii katika hayo humfanya mtu kumkubali Muumba Mtukufu Adhwimu, mwenye uwezo na mwenye hekima, na ya kuwa Maada haikuwa chochote isipokuwa kiumbe miongoni mwa viumbe wake vimetokea baada ya kuwa havikuwepo hapo kabla.

Mola huyu, mwenye hekima, mwenye uwezo ambaye amewajulisha waja wake na nafsi yake, na akawasimamishia alama na ishara za kuwepo kwake na dalili mbali mbali na fafanuzi mbali mbali, ambaye Yeye Allah anajitosha dhidi ya yote hayo (naye mwenyewe amejisifu kwa sifa kamilifu) sifa ambazo zinabainisha na kuthibitisha uwepo wake, Uungu wake, na Uola wake kwa sheria za mbinguni, na umuhimu wa kiakili na maumbile ya asili ya kitabia, na umma mbali mbali zikakubaliana katika hilo.

## Jibu lenye kutosheleza

"Historia ya dini kwa ujumla, na historia ya Tawhid haswa hutudhihirishia kuwa kumuamini Allah peke yake ni jibu tosha la kipekee la kila swali kuhusu ya Ulimwengu na ubinadamu na lengo la uwepo wao, haiwezekani maisha ya mwanadamu\yakawa na lengo ila Allah peke yake. Na kila ibada na dini kwa mwanadamu lengo lake ni asili ni iwe mtu anajua au hajui –humpelekea katika kumuamini Mungu mmoja."



**Cardinal Koenig**
Raisi wa Maaskofu wa Austria

https://www.path-2-happiness.com/sw

## DALILI NI ZIPI?



### 1. Kuwa Allah Ndiye Muangalizi wa yaliyomo katika ubunifu wa Uumbaji

-Je, huoni Ulimwengu huu Mkubwa na yaliyomo katika mbingu na ardhi?!

-Je, umefikiria hata siku moja kuhusu Uumbaji wa mbingu na yaliyomo katika sayari?!

-Je, hukuwahi kuwa na mazingatio katika ardhi ile na vilivyomo ndani yake katika mito, bahari, mabonde na milima?!

-Je, uratibu huu uliopangwa vizuri kwa ubunifu na ufanisi wa hali ya juu haujakufurahisha?.


-Je, ni nani aliyeumba Ulimwengu huu na ukawa katika hali hii ya ubunifu wa hali ya juu iliyopangiliwa kwa mpangilio wa juu kabisa na kupambwa katika umbile hili lenye muujiza kiasi cha kuwa ni alama na ishara ya ukamilifu, na katika isiyokuwa na mfano uliotangulia?!

-Je, ameiumba nafsi yake?! Au katika Ulimwengu huu kuna Muumba mwenye uwezo? Allah amesema: {Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili, Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto.} [3:190-191].

Je, haijawahi kukupitia akilini mwako siku moja kuhusu kuumbwa kwako? Allah amesema: {Na pia katika nafsi zenu - Je! Hamwoni?} [51:21]

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



**Mungu ni Kweli**

"Utakapofikiri kwa kina; Sayansi itakulazimisha kuamini kuwepo kwa Mungu."

**Lord Kelvin**

Mwanafizikia wa Scotland

Sasa ni vipi alivyoumbwa mwanadamu? Allah amesema: {Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji? Au wao wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana na yakini. } [52:35-36]

Na kama hakuumbwa hapo kabla alipokuwa si kitu, (achilia mbali kwamba wao hawakujiumba na kuumba nafsi zao, bali hawakuumba mbingu na ardhi), hakuna shaka yoyote kuwepo kwa Muumba wa Ulimwengu huu na vyote vilivyomo, nae si mwigine bali ni Allah Mtukuka, cha kushangaza mno ni ile hali wanaopinga kuwepo kwa Allah muumba, mwenye kusawiri kila kitu baada ya ishara zote na dalili mbali mbali!!

## 2. FITRA (MAUMBILE ASILI)

Kwa hakika viumbe wako katika fitra ya kukiri uwepo wa Allah Ta'ala bila ya shaka yoyote ile, kama vile ambavyo anavutika katika kupenda kheri na kuchukia mambo mabaya, bali bila ya shaka kukiri kwao uwepo wa muumba ni katika mambo makubwa yaliyomo na kudumu kwenye fitra kiasi cha kutohitaji dalili yoyote au uthibitisho wowote ule, Allah amesema: {Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilo waumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui. } [30:30]

Na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) naye akasema: «Hakuna mtoto anayezaliwa ila huzaliwa katika fitra» (Bukhari na Muslim)."

**Hisia za Kimaumbile**

"Mungu ambae tunajisalimisha kwa uwepo wake, haishii kwenye Ulimwengu wa Mada, wala hisia zetu dhaifu haziwezi kumdiriki (kumpata), na katika hilo ni mchezo kujaribu kuthibitisha uwepo wake kwa kutumia sayansi: kwa sababu Mungu mwenyewe huchukua duara lisilokuwa duara lake finyu lenye ukomo. Kwa hakika imani ya kuwepo Mwenyezi Mungu ni katika mambo mahususi ambayo yanaota katika hisia ya mwanadamu na dhamira yake na kukua katika mzunguko (duara) wa uzoefu wake binafsi."



**Robert Morris Page**

Mwanasayansi

https://www.path-2-happiness.com/sw

## 3. MAKUBALIANO YA UMMAH

Ummah mbali mbali zimeshakubaliana tokea zamani kunasibisha maumbile na uumbaji wa Ulimwengu huu kwa Allah Ta'ala hivyo kukawepo makubaliano– yaliyodumu ya kuwa Allah Ta'ala ndie muumba wa Ulimwengu huu bila ya mshirika, hivyo Ummah wote hauwezi kuacha kuzingatia kuwepo Muumba wa Mbingu na Ardhi, au Mruzuku asiyekuwa Allah Mtukuka, bali pindi wanapoulizwa kuhusu hayo hukiri (pamoja na ushirikina wao) ule Uungu wa Allah Ta'ala. Amesema Yeye mwenye shani; {Na ukiwauliza; Nani aliye umba mbingu na ardhi na akafanya jua na mwezi kuti'ii amri yake? Bila ya shaka, watasema: Mwenyezi Mungu. Wapi basi wanako geuzwa? Mwenyezi Mungu humkunjulia, na humdhikishia, riziki amtakaye katika waja wake. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.} [29: 61-63]

Na akasema vile vile: {Na ukiwauliza: Nani aliye ziumba mbingu na ardhi? Bila ya shaka watasema: Kaziumba Mwenye nguvu, Mjuzi} [43:9]

Ama hali ya watu kumkana Mwenyezi Mungu na kukufuru kwao Allah Ta'ala (kama ilivyotangulia kuelezea) ni hali ya kujitenga, yaani ni hali ya kujitenga wafuasi wake wa fikra hii ya kumkana Allah na kundi la watu wenye akili, na kukadhihirika kufeli kwa fikra hiyo katika uhalisia wake.



### Imani ya Mungu ni maumbile (Fitra)

"Akili zinazokuwa katika hali ya kawaida kwa watoto zinawafanya kuelekea katika kumuamini Mungu Muumba, badala ya makuzi ambayo sio ya kawaida ya akili za binadamu na ugumu wa kukubali na kudhibiti."

**Justin Barret**

Mtafiti katika chuo kikuu cha Oxford

https://www.path-2-happiness.com/sw




## 4. USHAHIDI WA AKILI

Kwa nyongeza ya yaliyotangulia katika dalili na ushahidi mbali mbali yakuwepo kwa Allah na Uungu wake; basi akili ya mtu ni miongoni mwa dalili kuwa ya kuwa Uumbaji huu wa Ulimwengu katika hali hii haiwezekani kabisa kuwa imejiumba yenyewe; yaani kiumbe kilichotokea tu na kuzuka na bila ya shaka yoyote kuwa kila chenye kuzuka hakikosi mzushaji.

Swali lenye kujitokeza hapa; ni mara ngapi umepata dhiki au msiba au lawama, umeelekea kwa nani? Umenyenyekea kwa nani? Nani umemuomba akuondoshee dhara yako na kufariji humumi na huzuni zako?! Allah Ta'ala amesema: {Na taabu inapo mfikia mtu humwomba Mola wake Mlezi naye ameelekea kwake. Kisha akimpa neema kutoka kwake, husahau yale aliyo kuwa akimwitia zamani, na akamfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili apoteze watu njia yake. Sema: Starehe na ukafiri wako kwa muda mchache. Kwani hakika wewe utakuwa miongoni mwa watu wa Motoni.}[39:8]

Katika aya nyinginezo Allah amesema, {Yeye ndiye anaye kuendesheni bara na baharini. Hata mnapo kuwa majahazini na yakawa yanakwenda nao kwa upepo mzuri wakaufurahia, upepo mkali ukawazukia, na yakawajia mawimbi kutoka kila upande, na wakaona wamesha zongwa, basi hapo humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia niya: Ukituokoa na haya bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa wanao shukuru. Lakini akisha waokoa, mara wanafanya jeuri tena katika nchi bila ya haki. Enyi watu! Jeuri zenu zitakudhuruni wenyewe. Hii ni starehe ya maisha ya dunia tu. Kisha marejeo yenu ni kwetu, na hapo tutakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda.}[10:22-23]



**Kuwa Mwenye Akili**

"Je, inawezekana mwenye akili kupima au kuamini kuwa mada tupu ya akili na hekima imejitengeneza yenyewe kwa kubahatisha tu"?!

**John Cleveland Cothran**

Profesa wa Sayansi katika Chuo Kikuu cha Dolth



### Falsafa na Dini

Falsafa kidogo inamsogeza mtu kwenye kumpinga Mungu. Ama kubobea katika Falsafa humrudisha mtu kwenye dini."

**Francis Becon**

Mwanafalsafa wa Uingereza

Na amesema vile vile, {Na wimbi linapo wafunika kama wingu, wao humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia dini. Lakini anapo waokoa wakafika nchi kavu, wapo baadhi yao huenda mwendo wa sawa. Wala hazikanushi Ishara zetu ila aliye khaini kafiri mkubwa.}[31:32].

## DALILI ZA UUNGU WA ALLAH TA'ALA

Maumbile sahihi na akili zilizotua zinakiri kuwa Ulimwengu huu una Mola, na Viumbe hivi vina Muumba; na vimethibitisha kuwepo kwa Uungu wake na ya kuwa Yeye ni Mmoja katika Uungu na Uola wake, hana mshirika katika Uungu wake, na dalili zake ni nyingi na zipo wazi, miongoni mwazo ni:

1. haiwezekani kuwepo na Miungu wawili katika Ulimwengu huu?!!

Lau kwamba kungekuwepo na miungu



https://www.path-2-happiness.com/sw

wawili (kwa ajili ya mjadala tu) swali litabakia: Vipi kama watapingana na kila mmoja kuekeleza matakwa yake?!! Mmoja akataka jambo na mwingine atake kinyume chake?!

haiwezekani ila mmoja kuwa juu ya mwingine, na hahesabiwi mwingine kuwa ni mnyonge au dhaifu, Je, mnyonge anaweza kuwa ni Mungu?!! Na kubakia Mungu kuwa ni mmoja tu, Allah Mtukuka amesema: {Mwenyezi Mungu hana mwana yeyote, wala hanaye mungu mwengine. Inge kuwa hivyo basi kila mungu angeli chukua alivyo umba, na baadhi yao wangeli washinda wengine. Mwenyezi Mungu ameepukana na sifa wanazo msifu. Mjuzi wa siri na dhaahiri, na ametukuka juu ya hayo wanayo mshirikisha nayo.}[23:91-92].

Cha kushangaza ni mtu kumuabudu asiye na uwezo wala nguvu, hana umiliki wa mbingu na ardhi, hawezi kuumba chochote, hamiliki chochote katika nafasi yake mbali ya kuwamilikisha wengine –madhara au manufaa, mauti wala uhai wala ufufuo Allah Ta'ala




**Hakuna Mungu ila Allah**

"Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.." (6:4).

**Agano la Kale (Torati)**

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



**Herschel**

Mwanafalsafa na Mtaalamu wa sayari wa Uingereza

## Upekee wa Mungu

"Kila wigo wa elimu unapopanuka huongezeka dalili na uthibitisho wa uwepo wa hekima ya Muumba mwenye uwezo usio na mipaka na wanazuoni wa ardhi, taasisi mbali mbali, sayansi ya mazingira halisi na hesabu hujitahidi katika tafiti na ugunduzi wao kila chenye kulazimu ili kuanzisha hekalu la elimu ili kunyanyua neno la Muumba."

amesema: {Ametukuka aliye teremsha Furqani kwa mja wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote. Ambaye ni wake ufalme wa mbingu na ardhi, wala hakuwa na mwana, wala hakuwa na mshirika katika ufalme, na akaumba kila kitu na akakikadiria kwa kipimo. Na wamechukua badala yake miungu ambayo haiumbi chochote, bali hiyo inaumbwa, haijimilikii nafsi zao madhara wala manufaa, wala haimiliki mauti, wala uhai, wala kufufuka.} [25:1-3].

Vinginevyo kama jambo ndilo kama wasemavyo washirikiana kuwa pamoja na Allah kuna miungu ambao huabudiwa ili kumkurubisha kwake aombewe basi hao waabudiwa wanamuabudu na wanajikurubisha kwake na kutafuta kwao wasila na ukuruba, Allah Ta'ala amesema: {Sema: Lau kuwa wangeli kuwa pamoja naye miungu mingine kama wasemavyo, basi wangeli tafuta njia ya kumfikia Mwenye Kiti cha Enzi. Subhanahu Wa Taa'la, Ametakasika na Ametukuka juu kabisa na hayo wanayo yasema. }[17:42-43],

Bali Yeye ni Allah mmoja Mkusudiwa, ambaye hakuzaa wala kuzaliwa wala hafanani na chochote.

Hawa wenye kuabudiwa hawamiliki chochote wala hawawezi; Allah amesema: {Sema: Waite mnao wadaia kuwa ni badala ya Mwenyezi Mungu. Hawamiliki hata uzito wa chembe hichi katika mbingu wala ardhi. Wala hawana ushirika wowote humo. Wala Yeye hana msaidizi miongoni mwao. Wala uombezi mbele yake hautafaa kitu, isipo kuwa kwa aliye mpa idhini.} [34:22-23]



https://www.path-2-happiness.com/sw

Yaani, Waambie washirikina wanaomshirikisha Allah na viumbe vingine ambao hawanufaishi wala hawadhuru, ambao hawana uwezo na, pamoja na udhaifu uliopo lakini bado wanashikamana nao, wabainishie ubatili wa ibada zao; Waombeni hao wanaodai kumshirikisha Allah, kama kweli maombi yenu yanawafaeni, kwani hakika kuna sababu za udhaifu na kushikamana kwao, na kutoweza kujibu dua kutoka popote, kama ni hivyo hawamiliki chochote; hawamiliki hata udogo wa mdudu chungu mbinguni wala ardhini kwa kujitenga au kwa kushirikiana katika hilo. Na Miungu ile ambao mnadai wapo mbinguni na ardhini ambayo mnamshirikisha kwayo Allah haina uwezo wa kumiliki chochote kile, si kidogo wala kingi. Miungu ile ya kishirikina haina ufalme wala ushiriki, labda isemwe: Huenda wakawa ni wasaidizi wa mfalme, na mawaziri wake, hivyo basi maombi yao huenda yakawa na manufaa; (kwa sababu Mfalme ana haja nao) basi atawatekelezea haja zao kwa wale waliokuwa nao karibu; na hilo Allah Ta'ala amelikana daraja hili kwa kusema: {ana nini}; yaani Allah ni mmoja Mtenza nguvu {miongoni mwao.} Yaani: kwa waabudiwa {msaidizi} yaani msaada na waziri ambao humsaidia katika ufalme wake na mipango yake.

Mwenye kuuangalia Ulimwengu huu na mwenendo wake ataona mpango uliopangika kwa utaratibu wa hali ya juu; na hii ni dalili ya kuwa kuna mwenye kuiendesha naye ni Mungu mmoja Mzuri Mwenye uwezo, amesema Ta'ala: {Na Mungu wenu ni Mungu mmoja tu, hapana mungu ila Yeye. Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na kukhitalifiana usiku na mchana, na marikebu ambazo hupita baharini kwa viwafaavyo watu, na maji anayo yateremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, na kwa hayo akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake, na akaeneza humo kila aina ya wanyama; na katika mabadiliko ya pepo, na mawingu yanayo amrishwa kupita baina ya mbingu na ardhi, bila shaka zimo Ishara kwa watu wanao zingatia. } [2:163-164].

Je, utaratibu huu haukuwa ukienda mwaka mzima wala haiharibiki wala kusimama sekunde moja jambo ambalo lingeharibu ulimwengu huu tulionao, yote hayo makadirio yake yako kwa Allah, Je, utaratibu haukuwa kutoka kwa Muumba mpangaji wa mambo mmoja, asiye na mshirika?! Je, hii si dalili ya wazi ya kutowezekana uwepo Uungu zaidi ya mmoja kwa mtu mwenye akili?! Allah Ta'ala amesema: {Lau wangeli kuwamo humo miungu wengine isipo kuwa Mwenyezi Mungu basi bila ya shaka hizo mbingu na ardhi zingeli fisidika. Subahana 'Llah Ametakasika Mwenyezi Mungu, Bwana wa A'rshi (Kiti cha Enzi), na hayo wanayo yazua.} [21:22].



https://www.path-2-happiness.com/sw


Yaani lau katika mbingu na ardhi kungekuwa na miungu wawili basi yangeharibika na kuharibika yaliyomo kwa viumbe, kwa hakika ulimwengu huu (kama inavyoonekana) katika ukamilifu utakavyokuwa katika islahi na kufuata utaratibu ambao hauna kasoro wala aibu yoyote, wala katazo, wala upinzani na hii inathibitisha kuwa mpangaji wake ni mmoja, na Mola ni mmoja na Mungu ni mmoja lau kama kungekuwa na wapangaji wawili na Mola wawili au zaidi ya hao; basi utaratibu wake ungeharibika, na nguzo zake zingebomoka basi bila ya shaka zingezuiana na kupingana, na kama mmoja wao angetaka kupanga kitu na mwingine hataki hilo, basi ingeshindikana wote kufanikiwa katika matakwa yao, na kufanikiwa kwa matakwa ya mmoja bila ya mwingine ni uthibitisho wa udhaifu wa mwingine, na kutokuwa na uwezo, na kukubaliana kwao na kuafikiana kwao katika jambo moja katika mambo yote ni jambo lisilowezekana; hivyo basi yapasa kwa mmoja mwenye nguvu na uwezo apate muradi wake peke yake bila ya kuzuiwa wala kupingwa na huyu ndie Allah Mmoja Pekee Mwenye nguvu na uwezo.



https://www.path-2-happiness.com/sw

## Lengo Kuu

"Ulimwengu huu umedhihiri kwetu kwa hali hii ambayo haijaacha kitu chochote cha kubahatisha, bali kila sehemu katika sehemu zake kuelekea kwenye lengo. Lengo hilo linaelekea kwenye lengo kuu kabisa kuliko hilo. Hivyo ndivyo inavyofikia katika lengo la mwisho."




**Plato**

Mwanafalsafa wa Kigiriki

Manabii wa wateule wote tokea zama za Adam ('Alayhi Salaam), hadi Nuuh, Ibrahim, Musa, Issa na Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) nao ni watu walioepushwa na madhambi ya nafsi zao na wenye akili angavu na kauli ya ukweli na amana ya kufikishana uongofu juu ya kumpwekesha Allah Ta'ala na kuwa Yeye ndiye Hapana Mungu ila Allah, Allah amesema: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu. } [21:25]

Na akasema vile vile kumsifu Nuhu ('Alayhi Salaam) {Tulimpeleka Nuhu kwa kaumu yake, naye akasema: Enyi kaumu yangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku iliyo kuu} [7:59]

Na akasema kuhusu Issa ('Alayhi Salaam) {Na hali Masihi mwenyewe alisema: Enyi Wana wa Israili! Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Kwani anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni. Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru.}[5:72]



Na akamuamrisha Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) awaambie watu wake: {Sema: Hakika imefunuliwa kwangu ya kwamba hakika Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Je! Mmesilimu?} [21:108]

Hivyo basi ni jambo la msingi kwa wenye akili nzuri kufuata Mtume wao, na kumpwekesha Allah Ta'ala na kumuamini Yeye Mola wao mlezi na Mungu wao, ili wapate furaha ya duniani na ya Akhera, Allah Ta'ala amesema: {Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda.} [16:97].

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



Kwa hakika matendo mema pamoja na imani malipo yake ni maisha mazuri katika ardhi hii, sio lazima yawe ni yenye neema sana au utajiri wa mali, bali inaweza kuwa hivyo au isiwe hivyo, na maisha yanaweza kuwa mazuri lakini mtu bila ya kuwa na mali au utajiri; Katika maisha kuna mambo mengi ambayo sio mali wala utajiri, bali baadhi ya mambo ambayo mtu katika maisha yake anayafurahia, ni kama:-

i-Mawasiliano ya mtu na Mola wake, kumuamini na kuwa na utulivu na ulezi wake na stara yake, na kuridhiwa naye.

ii-Kuna suala la afya ya mtu na utulivu wake, kuridhika na kupata baraka, kuishi katika nyumba na mapenzi katika mioyo.

iii-Kuna suala la mtu kufurahi kwa kufanya kwake matendo mema na athari yake katika dhamira yake, na katika maisha yake, Na hayakuwa mali katika maisha ya mwanadamu isipokuwa ni kipengele kimoja tu katika pambo katika maisha yake: {Mali na wana ni pambo la maisha ya dunia. Na mema yanayo bakia ni bora mbele ya Mola wako Mlezi kwa malipo, na bora kwa matumaini.} [18:46].

Itakapokuwa moyo wa mwanadamu unaungana na kitu kilichokuwa kitukufu zaidi na chenye kubaki zaidi kwa Allah Ta'ala basi wakati huo maisha ya mtu huyo yanakuwa na maana nyingine, na furaha hali kadhalika inakuwa na maana nyingine katika maisha.

Mwanadamu huyo akikataa ila kuipa mgongo, basi atakuwa ameiridhia nafsi yake njia nyingi za tabu na balaa ambazo kupata mara kwa mara bila kukatika, na huenda mtu huyo akawa ameridhia nafsi yake njia nyingi za tabu na shida na mashaka anaelea hapo bila kuacha, Allah Ta'ala amesema:

### Bwana Mmoja

"Wewe umeonyeshwa haya, ili upate kujua ya kuwa BWANA ndiye Mungu, hapana mwingine ila yeye" (Kumbukumbu la Torati) 4:35).
"Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine zaidi yangu mimi hapana Mungu." (Isaya 45:5).


### Mungu Mmoja

"Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani, kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake." (Mathayo 4:10, Luka 4:8).
"Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma." (Yohana 17:3).

Agano Jipya (Injili)

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



## Dalili ya Furaha

"Sikujua furaha hapo kabla. Tokea nianze kusoma Qur-aan nami nilijiuliza hali ninashangaa, kwanini watu wanakwenda bila muongozo kwenye dunia hii hali ya kuwa dalili na mwanga ipo mbele yao."?!

**Cat Stephens (Kwa sasa Yusuf Islam**

Aliyekuwa Muimbaji wa Uingereza

{Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumhidi humfungulia kifua chake kwa Uislamu. Na anaye taka apotee hukifanya kifua chake kina dhiki, kimebana, kama kwamba anapanda mbinguni. Namna hivi Mwenyezi Mungu anajaalia uchafu juu ya wasio amini.} [6:125],

Atakaye mpwekesha Mwenyezi Mungu mmoja bila ya kumshirikisha basi mtu huyo atakuwa na moyo uliofunguka na raha na utulivu.

Ama yule aliyempoteza anaufanya moyo wake una dhiki, tabu na kero, Allah atulinde, naye ni mfano wa aliyeamini na kumpwekesha Allah pekee, na yule ambae amemshirikisha Mwenyezi Mungu na kupotea, Mwenyezi Mungu ametoa mfano mwingine; aliposema: {Mwenyezi Mungu amepiga mfano wa mtu mwenye mabwana washirika wanao gombana, na wa mtu mwengine aliye khusika na bwana mmoja tu. Je! Wako sawa katika hali zao? Alhamdulillahi, Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu! Lakini wengi wao hawajui.} [39:29].

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw


Mtu mshirikina ni kama vile mtu anamilikiwa na idadi ya watu wenye tabia mbaya nao wanashindana, mmoja anamwambia njoo, na mwingine anamwambia kaa, na mtu wa tatu anamwambia simama; mtu huyu anababaika katika jambo lake hana raha ya kiwiliwili wala hana raha ya dhamira yake au nafsi yake, na mwenye kumpwekesha Allah ni kama vile mtu aliyehusika na bwana mmoja tu, angemwamrisha na kumkataza ni mtu mmoja tu, Je, watu hawa wawili wanalingana?! Alhamdulillah, shukran na himidi ni zake Allah pekee, na kusifiwa kuzuri ni kwake, na kuwa Yeye hapana Mola isipokuwa Yeye tu, ama wale ambao hawafahamu wanaishi maisha ya taabu na migongano ya ndani na yanayosuhubiana nayo miongoni mwa tabu na kero na sononeko na babaiko, mgongano na kujiuwa.



https://www.path-2-happiness.com/sw

## Kujiua na Dini

Wataalamu wawili kutoka katika Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) Dr. Jos Manuel na Mtafiti Alesandra Fishman wameainisha uhusiano kati ya kujiua na Dini anayofuata mtu, matokeo yalikuwa kama ifuatavyo: Katika utafiti wao wa kisayansi uliohifadhiwa katika marejeo ya Umoja wa Mataifa.
A global perspective in theepidemiology of suicide




https://www.path-2-happiness.com/sw